ISSN 0856 - 034X

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

***Supplement No. 46*** ***2nd December, 2022***

***SUBSIDIARY LEGISLATION***

*To The Gazette of the United Republic of Tanzania No. 47 Vol. 103 Dated 2nd December, 2022*
Printed by The Government Printer, Dodoma by Order of Government

TANGAZO LA SERIKALI NA. 692 la tarehe 2/12/2022

SHERIA YA MIPANGOMIJI,

(SURA YA 355)

# AMRI

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 8(1))*

AMRI YA KUPANGA ENEO LA UHURU YA MWAKA, 2022

Jina

1. Amri hii itajulikana kama Amri ya Kupanga Eneo la Uhuru ya Mwaka, 2022.

Kutangazwa kwa eneo la upangaji Sura ya 355

2. Eneo lililoainishwa katika Jedwali la Amri hii linatangazwa kuwa eneo la upangaji kwa madhumuni ya Sheria ya Mipangomiji.

Mpango wa jumla na kina wa eneo

3. Mpango wa jumla na wa kina wa eneo lililoainishwa katika Jedwali unaandaliwa na kuhifadhiwa kwa Mkurugenzi wa Mipangomiji na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Urambo.

**JEDWALI**

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 2)*

Eneo la Upangaji lipo ndani ya mipaka ifuatayo:

“Unaanzia kwenye alama ya mpaka ya upimaji U1 iliyopo barabara ya Kigoma Magharibi mwa makazi ya Uhuru yenye majira-nukta 373990E, 9438234N; baada ya hapo mpaka utaelekea Kusini - Mashariki katika uelekeo wa S170$^{0}$11’20”E kwa umbali wa kilomita 1.7 hadi alama ya mpaka ya upimaji U2 yenye majira - nukta 374351E, 9436588N; baada ya hapo mpaka utaelekea Mashariki - Kaskazini katika uelekeo wa E70$^{0}$4’40”N kwa umbali wa kilomita 3.9 hadi alama ya mpaka ya upimaji U3 iliyopo barabara ya nyenze yenye majira-nukta 378225E, 9438409N; baada ya hapo mpaka utaelekea Kaskazini - Mashariki katika uelekeo wa N105$^{0}$7’0” kwa umbali wa kilomita 2 hadi alama ya mpaka ya upimaji U4 iliyopo barabara ya Kigoma Mashariki mwa makazi ya Uhuru yenye majira-nukta 378571E, 9440340N; baada ya hapo mpaka utaelekea Kaskazini - Magharibi katika uelekeo wa N175$^{0}$11’40” kwa umbali wa kilomita 0.6 hadi alama ya mpaka ya upimaji U5 iliyopo reli ya Kigoma yenye majira-nukta 378434E, 9440921N; baada ya hapo mpaka utafuata reli ya Kigoma hadi alama ya mpaka ya upimaji U6 yenye majira-nukta 374430E, 9440457E; baada ya hapo mpaka utaelekea Kusini - Magharibi katika uelekeo wa S87$^{0}$5’48” kwa umbali wa kilomita 2.2 hadi ulipoanzia”

Dodoma,
8 Novemba, 2022

ANGELINE S. MABULA
*Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi*